

LEARNING BY EAR

"If a tree falls... - Deforestation in Africa"

EPISODE FIVE: "Timber and Conservation"

AUTHOR: Romie Singh

EDITORS: Thomas Mösch, Jan-Philipp Scholz

PROOFREADING: Natalie Glanville-Wallis

List of characters EPISODE FIVE:

Narrator

SCENE 1 Akiki (f, 7)

SCENE 2 Akiki (f, 7) Chika (f, 18) Isi (m, 18)

SCENE 3 Chika (f, 18) Isi (m, 18)

SCENE 4 Mulogo (m, 22) Chika (f, 18) Isi (m, 18)

SCENE 5 Chief (m, 40)

SCENE 6 Chief (m, 40) Mother (f, 36)

SCENE 7 Akiki (f, 7)

INTRO

Karibu kwenye *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* na katika kipindi cha tano cha mchezo wetu mpya kuhusu uharibifu wa misitu.

Kisa hiki kinaendelea kwenye mazingira ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na kinaonyesha jinsi uharibifu wa misitu- ukataji wa miti na maeneo ya nyasi- ulivyotatiza maisha ya vijijini na kusababisha mzozo kati ya jamii mbili za wakulima. Sasa jamii hizo mbili zinajikuta ziko pamoja kwenye kambi ya wakimbizi ya Dovani na zimeanza kutafuta ufumbuzi sawa kwa matatizo ya siku zijazo.

Katika kipindi cha leo, viongozi wa kambi ya Dovani, Talib na Chika, wanashirikiana na jamii kutatua matatizo ya upungufu wa kuni na maji. Wakati huo huo, Mulogo anajitahidi awezavyo kuwa karibu na Chika. Jiunge nasi sasa usikie jinsi Chika anavyoamua kutumia uzoefu wa kuongoza wa Mulogo na Isingoma kusaidia kuhifadhi misitu.

Episode FIVE: "Timber and Conservation."

1.MUSIC UP

Scene 1

2.AKIKI NARRATOR: Mimi na Isi hatujazungumza lolote leo. Sote tumesikitika kwamba hakuna jamaa yetu yeyote aliyekuja kwa lori jana usiku. Nilitaraji kuwaona mamangu, babangu, na dadangu mkubwa, Sesi. Na Isi aliamini kwamba Kato alikuwa kwenye lori. Hakuna mtu hata mmoja tunayemjua aliyekuwa kwenye lori hilo. Inasikitisha si haba.

Scene 2

3. SFX Footsteps approaching. FADE IN Daytime ambience outside

- 4.AKIKI:** Chika huyo anakuja. Nadhani anataka kutuchangamsha.
- 5.CHIKA: (gently)** Akiki hujambo. Unaonekana mwenye huzuni.
- 6.AKIKI: (softly)** Hmmm. Sijambo Chika.
- 7.CHIKA:** Mambo vipi Isi. Ninakushuru sana kwa kunisaidia kuwasajili watu waliokuja jana usiku.
- 8.ISI: (depressed and quiet)** Si Neno.
- 9.CHIKA:** Sikiza! Ninakwenda kupiga mguu pamoja na Mulogo. Ungetaka kujiunga nasi? Nadhani anataka sana tubadilishane mawazo na ni vyema na wewe pia uwepo.
- 10.ISI:** Na Akiki je?
- 11.CHIKA:** Akiki, Natumai huna neno tukikuacha kwa muda wa sasa chache!
- 12.AKIKI:** Hata! Sina neno. Ninafurahia kuchunga ng'ombe. Nenda Isi. Sina neno.

13.ISI: (softly) Haya. Tutaonana baadaye.

Scene 3

14. SFX Forest sounds. Footsteps through leaves

15.ISI: Mbona usiende peke yako Chika. Anaonekana kwamba anakupenda!

16.CHIKA: Alaa, kumbe ushaona!

17.ISI: Pengine kipofu ndiye asiyeona!

18.CHIKA: Hapana, tafadhali Isi usende. Nataka kufanya kazi kwa bidii. Wewe na Mulogo mtakuwa watu muhimu sana katika jamii zetu. Ni suala la uongozi. Mnapaswa kuhusishwa.

19.ISI: Mimi pia ninaridhia. Tutumaini kwamba Mulogo atashirikiana nasi!

20.CHIKA: Acha nikutanabahishe: Tumekuwa tukijadiliana mambo machache: mabadiliko ya hali ya hewa, na kama tunapaswa kuwahamasisha watu kuhama kwenye misitu wakaishi mijini, au ikiwa tunaweza kuendelea haraka tukikata miti na kujenga maeneo mengi ya miji. Mambo kama hayo.

21.ISI: Nadhani Mulogo amechanganyikiwa. Hana ufumbuzi wa suala la mabadiliko ya hali ya hewa. Anataka kubaki hivyo kama kwamba hakuna lolote linalotendeka duniani. Maziwa yetu makubwa zaidi barani Afrika yanakauka huku akizungumza kuhusu ujenzi wa mtambo wa nguvu za umeme. Mawazo yake hayo hayafai.

22.CHIKA: (gently) Hayo ni matatizo mazito yanayotaka ufumbuzi wa kina. Usimwendeshe mbio sana. Anajifanya mjuvi!

Scene 4

23. SFX Forest ambience

24.MULOGO: (approaching OFF MIC) Hujambo Chika. (Surprised)

Alaa! Isi hujambo.

(ON MIC whispering) Kwa hivyo Chika umeamua hutaki kwenda kutembea mwituni nami eeh!

25.CHIKA: (Whispering) Hapana! Si jambo zuri. Sote watatu tunaweza kutembea pamoja huku tukizungumza.

26.MULOGO: (grumpy) Hmmmm.

27.CHIKA: (Normal voice) Haya. Tuanzie hapa. Tazama miti hii ya mibambakofi. Tazama urefu wake, jinsi ilivyo laini na matawi yake juu.

28.ISI: Inapendeza.

29.MULOGO: Na ina thamani sana. Na hiyo ndiyo hoja yangu. Sisi waafrika tunahitaji fedha za kuendeleza uchumi wetu. Wazungu wako tayari kulipa fedha chungu nzima kununua miti hii migumu.

30.CHIKA: Haya, kwa hivyo tuikate. Kisha baadaye? Itakuwa muda kiasi gani kwa miti mingine kama hii kukua ili tuendeleze biashara?

31.MULOGO: Tunaweza kuendelea kupanda mingine. Nadhani mti mmoja huchukua miaka kumi kukua. Kweli?

32.CHIKA: Kiasi kama hicho, kweli. Kwa hivyo unataka eneo ambalo limetengewa miti ya mbao, sivyo? Kukata kisha kupanda miti mingine msituni.

33.MULOGO: Naam.

34.CHIKA: Basi, tuna maeneo ya msitu ambayo yametengwa – maeneo ambayo miti hukatwa kulingana na mipango ya Idara ya Msitu..

- 35.ISI:** Nadhani wana muda wa miaka mitano ya kukata miti kisha miaka mitano mingine bila kukata miti. Lakini nilisikia kwamba mwitu unahitaji miaka mia moja kurejea hali yake ya zamani.
- 36.CHIKA:** Naam...kweli usemayo, kwa sababu hatua ya kukata miti husababisha mazingira ambayo miti hiyo hukulia. Ndio sababu miti inahitaji muda mrefu... miti hiyo inatakikana kuzoea hali tofauti.
- 37.ISI:** Miti inasikizana na mazingira na ndio sababu unaona baadhi ya miti katika maeneo fulani na si maeneo mengine. Kwa hivyo kwa miti kuzoea hali mpya ya hewa inachukuwa muda mrefu- pengine vizazi kadha.
- 38.MULOGO:** Lakini tuna maeneo makubwa sana ya misitu. Tunaweza kutumia baadhi ya misitu hiyo.
- 39.CHIKA:** Tayari tumepoteza misitu. Mulogo, kwa hisani yako, **(Slowly and clearly)** Bara la Afrika ndilo la pili kwa kasi ya kupoteza maeneo ya misitu ULIMWENGUNI. Hekta milioni tatu nukta nne KILA MWAKA. Eneo hili ni kubwa kuliko eneo la nchi ndogo kama vile Rwanda.
- 40.MULOGO:** Sawa! Sawa! Tulia. **(Whispering)** Isi...Unaonaje macho yake anapokasirika?
- 41.CHIKA: (angry)** Mulogo tafadhali! Usinikosee adabu!
- 42.MULOGO (Shocked)** Samahani Chika! Ninakutania tu! Samahani. Sawa. Tuendeleo! Sasa...kwa nini tusikate miti migumu ambayo tunaweza kuuza mataifa ya nje. Tunapaswa kuondokana na umaskini.

43.ISI: Watu wanaweza kuondokana na umaskini kwa kufuata mbinu nzuri za kilimo na upandaji miti. Turejeelee wazo lako....utawezaje kukata tu miti migumu? Unaona yote imekaribiana sana.

44.CHIKA: Na kuna maelfu ya aina za miti mwituni. Wenye makampuni ya mbao watakwambia kwamba ni vigumu sana kupata miti mwafaka ya kukata..

45.MULOGO: (irritated) Aaakh! Nyote hamna jema msemalo.

46.CHIKA: Sasa? Je unaona mahala ambapo ni pa mibambakofi pekee mwituni? Eeh? Hapana! Kwa nini? Kwa sababu kuna miti aina nyingi: mikafuri, mikalitusi, mibambakofi na kadhalika. Kuna aina nyingi za miti ambazo makampuni ya mbao yangetaka kufikia mwituni,lakini wao hufikia chache sana- kwa sababu mwitu ni mkubwa na umejazana miti.

47.ISI: Hmm. Si rahisi kama unavyofikiria, Mulogo; Si rahisi kwa kweli.

48.MUSIC UP

Scene 5

49.CHIEF APALOO NARRATOR: Katika eneo la kusini mashariki.

Mwitu wa Miombo ulikuwa ukienea katika sehemu kubwa na pia ulikuwa makazi ya ndege wa kuvutia pamoja na wanyama pori. Lakini wakati majirani zetu wa jamii ya Banega walipoanza kukata miistu, ndege hao walitoweka. Ndovu pia, punda milia na paa– wote wametoweka.

Mimi nikiwa Chifu wa Wilaya ya Abanto nimejaribu kuhifadhi misitu na kutafuta mbinu za kutumia vyema kuni na makaa. Nimekuwa nikitafuta mbinu za kupunguza matumizi ya kuni. Nilivumbua "Jiko la kombora!" Kusema la haki si uvumbuzi wangu. Hata hivyo ninajua jinsi ya kuliunda! Talib amelipenda sana! Sasa lililobaki kuwashawishi kina mama!

Scene 6

50. SFX Daytime ambience.

51.CHIEFAPALOO: Bi Kipko! Ninakushukuru sana kwa kupata muda wa kukutana nami!

52.MOTHER: Chifu Apaloo. Karibu nyumbani kwangu. Nafurahi kwamba umefika kwangu.

53.CHIEF APALOO: Unaendeleaje?

54.MOTHER: Aaah...Salama. Nina furaha sana hapa nyumbani kwangu.

55.CHIEF APALOO: Vizuri hivyo. Una habari za mumeo, Chifu Kipko?

56.MOTHER: Hapana, lakini asante kwa kuuliza. Yeye na wanangu wawili hawajulikani waliko, Jamal na Kato, pacha mwenzake Isi.

57.CHIEF APALOO: (embarrassed) Pole sana! Ninasikitika. Mimi na mume hatukuwa tukipatana. Nadhani unajua hayo. Tulikorofishana. Lakini hali sasa imebadilika. Natumai yeye na wanao watarejea salama.

58.MOTHER: Naomba hivyo. Hata hivyo vita hivi vimeleta uzuri wa kuunganisha jamii mbili mahasimu! Tumekuwa katika kambi ya Dovani kwa zaidi ya miezi sita. Hatimaye mimi na wewe tumekutana!

59.CHIEF APALOO: Ndivyo tulivyo, sisi Waafrika! Kila jambo na wakati wake.

60.MOTHER: Naam. Ngoja nikuandalie kikombe cha chai.

61.CHIEF APALOO: Haya! Nimeyajia hayo. Sasa hivi nitakuonyesha jinsi ya kutumia jiko langu jipya. Tafadhali! Litumie kupika chai uone jinsi linavyofanya kazi.

62. SFX: Putting stove down

63.MOTHER: Alaa! Hili ni jiko? Linafanana na kombora!

64.CHIEF APALOO: Linapata joto haraka kama kombora – tena linapata joto kwa kasi. Utahitaji tu vijiti vitatu na nyasi kavu. Subiri nikusaidie!

65. SFX: Grass, sticks lighting of match

66.MOTHER: Ajabu- Moshi utokao ni mdogo sana. Ina maana jiko hili linafaa sana ndani ya nyumba. Na hili shubaka la vyuma ni la nini?

67.CHIEF: Ninaliweka hivi...

68. SFX metal rack pushing on sand... mbele ya tundu hili kubwa. Kisha ninaweka vijiti vikubwa juu ili zifikiwe na moto kutokea tundu hili. Si vijiti vingi- vitatu au vinne vinatosha.

69.MOTHER: Vyema hivyo. Mimi huhitaji kiasi mara mbili cha kuni kama hizo.

70.CHIEF APALOO: Ndio hivyo.

71.MOTHER: Nadhani ni lazima tukualike uje utuonyeshe jiko hili katika mkutano wa kina mama kesho.

72.CHIEF: Kusema kweli Bibi Kipko, nilitaraji utafanya hivyo. Nadhani unaweza kueleza vyema zaidi yangu mimi. Kuna uwezekano kwamba kina mama watakuzingatia zaidi yangu mimi mwanamume mzee!

73.MOTHER: Chifu Apaloo! Wewe si mzee!

74.CHIEF APALOO: (Laughing) Hivyo ndivyo Talib alivyosema. Lakini anasema pia sisi machifu tunapenda maisha ya starehe kila kutwa!

75.MOTHER: Hayo ni kweli. Sisi kina mama tunapaswa kujiamini na kueleza vitu tunavyohitaji. Haya nitafanya hivyo. Siamini macho yangu!

76. SFX: Water Boiling

77. MOTHER: Maji tayari yanachemka.

78.CHIEF: Sasa unaweza kuvivunja vijiti, viache katika shubaka ili uvitumie mara nyingine. Makaa bado yanawaka ndani. Unaona umetumia nusu ya kuni!

79.MOTHER: Unaweza kuitengenezea kila nyumba jiko moja? Ebu kisia kiasi cha kuni ambazo tungehifadhi!

80.CHIEF APALOO: (triumphantly) Huo ndio mpango walio nao Talib na Chika! Waulize! Hata hivyo nasema inawezekana!!

81.MUSIC UP

Scene 7

82.SFX evening sounds/cows

83. AKIKI: (talking softly to her cow) Kiroko, rafiki yangu mwenye pembe. Niambie la kufanya. Ninajua jambo ambalo Isi hana habari nalo. Nilimwona ndugu yake Kato na dadangu Sesi wakitowekea mwituni, saa chache kabla ya wanajeshi wa waasi kufika. Walikuwa wakikutana kisiri. Siku moja niliwafuata. Walikuwa na mahali pa kujificha mwituni. Nadhani walikuwa na uhusiano – unajua Kiroko..uhusiano wa kimapenzi. Je nimwarifu Isi? Itafaa nini? Eeeh Kiroko? Itafaa nini? Na je kama wote wamefariki? Nitaiacha iwe siri yao.

84. AKIKI hums the same sad song Isi usually hums

85. MUSIC UP

OUTRO.

Ni hayo tuliyokuandalia kwa leo katika kipindi cha *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* kiitwacho "Mti unapoanguka...", kilichoandikwa na Romie Singh, kinachoshughulikia suala la uharibifu wa misitu.

Katika kipindi chetu kijacho, kina mama wanajifunza jinsi ya kupanda mimea ya mazao kutegemeana na udongo na pia misimu. Na Akiki ana ndoto- je ni dalili fulani?

Usikose kujiunga nasi katika kipindi cha sita upate kujua mambo yatakavyokuwa.

Kumbuka, ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaarifu marafiki zako kukihusu, tafadhali tazama wavuti wetu www.dw-world.de/lbe

Kwaheri kwa sasa!

END OF EPISODE 5